

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA
MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

636

TEHAMA

Muda: Saa 3

Mwaka: 2022

Maelekezo

1. Karatasi hii ina sehemu A na B zenye jumla ya maswali **kumi na nne (14)**.
2. Jibu maswali **yote**.
3. Sehemu A ina alama **arobaini (40)** na sehemu B ina alama **sitini (60)**.
4. Soma maelekezo **yote** yaliyopo katika kijitabu cha kujibia
5. Vifaa vya mawasiliano na vitu vyote visivyoruhusiwa **havitakiwi** ndani ya chumba cha mtihani.
6. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.



SEHEMU A (Alama 40)

Jibu maswali yote katika sehemu hii.

1. Moja kati ya njia za mawasiliano ni matumizi ya alama mbalimbali za barabarani. Fafanua mambo manne yanayoonesha umuhimu wa uwepo wa alama hizo.
2. Kuna tofauti gani katika utoaji wa habari kati ya njia ya redio na televisheni? Chambua kwa kifupi tofauti nne.
3. Maktaba ni kati ya sehemu muhimu ambako wadau mbalimbali wanaweza kwenda kupata ujuzi na maarifa mbalimbali. Ainisha wanufaika wanne wa sehemu hiyo katika jamii na jinsi wanavyonufaika na huduma zake.
4. "Rejesta ni njia ya uhakika zaidi ya utumaji wa barua na vifurushi." Unga mkono kauli hii kwa kueleza kwa ufupi sababu nne.
5. Ili matumizi ya kompyuta kama kifaa cha mawasilino yatimie, moja ya namna ya kufanikisha hilo ni kuunganisha kompyuta hizo katika mtandao. Elezea kwa kifupi vifaa muhimu vinne vinavyohitajika katika uunganishaji wa mtandao huo.
6. Kwa mujibu wa taaluma ya ualimu, upimaji unaweza kugawanywa katika aina kuu nne. Eleza kwa kifupi dhumuni la kila aina katika kupima maendeleo ya mwanafunzi katika somo la TEHAMA.
7. Ufundishaji na ujifunzaji unaweza kusaidiwa na teknolojia za aina mbalimbali zikiwemo redio, telesheni, simu ya mkononi na magazeti. Kwa kutoa hoja moja kwa kila aina, eleza kwa kifupi namna ambavyo mwalimu wa somo la TEHAMA anaweza kutumia teknolojia hizo katika kufundisha mada ya "Kuelezea kwa Usahihi Habari Iliyosemwa."
8. Katika kufanya maandalizi ya ufundishaji na ujifunzaji wa somo la TEHAMA, moja ya nyaraka muhimu katika maandalizi hayo ni Azimio la Kazi. Ainisha zana nne anazotakiwa kuwa nazo mwalimu wa somo la TEHAMA wakati wa maandalizi ya nyaraka hiyo.
9. Fikiria umepewa kazi ya kufundisha somo la TEHAMA, changanua kwa kifupi zana nne zinazoweza kutumika katika kufundishia mada ya huduma za posta.
10. TEHAMA kama yalivyo masomo mengine linaweza kukumbwa na uhaba wa zana za kufundishia na kujifunzia. Eleza kwa kifupi njia nne anazoweza kutumia mwalimu wa somo hilo kukabiliana na changamoto ya upungufu wa zana za kufundishia.

SEHEMU B (Alama 60)

Jibu maswali yote katika sehemu hii.

11. "Pamoja na ukweli kuwa maktaba zina utaratibu na kanuni zake, zipo kanuni ambazo ni za jumla ambazo kila maktaba inazingatia." Eleza kwa ufasaha kanuni tano za jumla ambazo kila maktaba husisitiza.
12. Mojawapo ya misingi ya ufundishaji wa somo la TEHAMA ni msingi unaozingatia usawa wa kijinsia. Eleza viashiria vitano vinavyoweza kuonesha kuwa msingi huo hauzingatiwi na mwalimu wakati wa ufundishaji na ujifunzaji wa somo hilo.
13. Kwa kutoa mifano, fafania madhara matano atakayopata mwalimu wa somo la TEHAMA iwapo atafundisha bila kuandaa Azimio la Kazi.
14. "Matumizi ya vitu halisi katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la TEHAMA huleta ufanisi mkubwa." Tetea kauli hii kwa kutumia hoja tano.